




JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA  
TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA



*Dar es Salaam, 25 Agosti, 2023*

## TAARIFA KWA UMMA

### KUKAMILIKA KWA AWAMU YA KWANZA NA KUFUNGULIWA KWA AWAMU YA PILI YA UDAHILI WA SHAHADA YA KWANZA KWA MWAKA WA MASOMO 2023/2024

#### 1.0 KUKAMILIKA KWA AWAMU YA KWANZA YA UDAHILI 2023/2024

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) inapenda kufahamisha umma, Taasisi za Elimu ya Juu na wadau wa Elimu ya Juu ndani na nje ya Tanzania kuwa Awamu ya Kwanza ya udahili wa Shahada ya Kwanza katika Taasisi za Elimu ya Juu nchini kwa mwaka wa masomo 2023/2024 imekamilika. Majina ya waliodahiliwa katika awamu hii yanatangazwa na vyuo husika.

Katika Awamu ya Kwanza ya udahili, jumla ya waombaji **116,133** wametuma maombi ya kujiunga katika vyuo **80** vilivyoidhinishwa kudahili wanafunzi katika Shahada ya Kwanza. Aidha, jumla ya programu **809** zimeruhusiwa kudahili ikilinganishwa na programu **757** mwaka 2022/2023 ikiwa ni ongezeko la programu **52** za masomo. Vilevile kwa upande wa nafasi za udahili, mwaka huu kuna jumla ya nafasi **186,289** ikilinganishwa na nafasi **172,168** mwaka uliopita. Hili ni ongezeko la nafasi **14,121** sawa na asilimia **8.2** katika programu za Shahada ya Kwanza.

Pia katika Awamu ya Kwanza ya udahili, jumla ya waombaji **86,624** sawa na asilimia **74.6** ya waombaji wote walioomba udahili wamepata udahili kwenye vyuo walivyoomba. Mwenendo wa udahili wa Awamu ya Kwanza kwa kipindi cha miaka mitano (2019/2020 hadi 2023/2024) unaonesha ongezeko la waombaji wenye sifa ya Kidato cha Sita na wale wa Stashahada.

Idadi ya waliodahiliwa katika Awamu ya Kwanza ya Udahili kwa kipindi cha miaka mitano (2019/2020 hadi 2023/2024) nayo imekuwa ikiongezeka. Mchanganuo wa mwenendo wa udahili kwa Awamu za Kwanza kwa kipindi cha miaka mitano umeainishwa katika **Jedwali Na.1**.

**Jedwali Na. 1: Mwenendo wa udahili kwa Awamu ya Kwanza kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2019/2020 hadi 2023/2024**

Na.	Maelezo	Idadi kwa mwaka wa masomo				
		2019/20	2020/21	2021/22	2022/23	2023/24
1	Jumla ya waombaji	83,197	90,572	92,809	106,295	116,133
2	Waliodahiliwa	51,385	60,621	68,019	75,163	86,624
3	Wasiudahiliwa	31,812	29,951	24,790	31,132	29,509
4	Waliodahiliwa chuo kimoja	30,527	32,120	32,471	38,157	43,411
5	Waliodahiliwa zaidi ya chuo kimoja	20,858	28,501	35,548	37,006	43,213

**2.0 WAOMBAJI WALIODAHILIWA KATIKA CHUO ZAIDI YA KIMOJA**

Waombaji waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja wanahimizwa **kuthibitisha** udahili wao katika chuo kimojawapo **kuanzia leo tarehe 25 Agosti hadi 06 Septemba, 2023** kwa kutumia namba maalum ya siri iliyotumwa kwa ujumbe mfupi kupitia namba zao za simu au barua pepe walizotumia wakati wa kuomba udahili. Wale ambao hawatapata kwa wakati ujumbe huo, wanashauriwa kuingia kwenye mifumo ya udahili ya vyuo walivyodahiliwa na kuomba kutumiwa ujumbe mfupi wenye namba maalum ya siri ili kuweza kujithibitisha katika chuo husika.

Aidha, inasisitizwa kuwa uthibitisho wa udahili ufanyike kupitia akaunti ambayo muombaji alitumia wakati wa kuomba udahili. Orodha ya majina ya waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja imewekwa kwenye tovuti ya TCU ([www.tcu.go.tz](http://www.tcu.go.tz)).

**3.0 KUFUNGULIWA KWA AWAMU YA PILI YA UDAHILI 2023/2024**

**Tume inatangaza kuwa Awamu ya Pili ya udahili wa Shahada ya Kwanza kwa mwaka wa masomo 2023/2024 imeanza leo tarehe 25 Agosti hadi 06 Septemba, 2023.** Tume inasisitiza kuwa waombaji ambao hawakuweza kutuma maombi ya udahili au hawakuweza kupata nafasi za kudahiliwa katika Awamu ya Kwanza kutokana na sababu mbalimbali, watumie fursa hii vizuri kwa kutuma maombi yao ya udahili kwenye vyuo wanavyovipenda.

Aidha, Tume inaelekeza Taasisi za Elimu ya Juu nchini kutangaza programu ambazo bado zina nafasi. Waombaji udahili na vyuo wanahimizwa kuzingatia utaratibu wa udahili wa Awamu ya Pili kama ilivyooneshwa kwenye kalenda ya udahili iliyoko katika tovuti ya TCU ([www.tcu.go.tz](http://www.tcu.go.tz)).

#### 4.0 WITO KWA WAOMBAJI UDAHILI

Waombaji udahili wa Shahada ya Kwanza wanakumbushwa kuwa masuala yote yanayohusu udahili au kujithibitisha katika chuo kimoja yawasilishwe moja kwa moja kwenye vyuo husika. Kwa wale ambao watapata changamoto katika kujithibitisha, vyuo vyote vimeelekezwa kupokea taarifa zao na kutafuta ufumbuzi wa haraka kwa kuzingatia miongozo na taratibu zilizowekwa.

#### 5.0 TAHADHARI

TCU inawaasa wananchi kuepuka kutapeliwa na watu wanaojiita mawakala au washauri wanaodai wanatoa huduma ya jinsi ya kujiunga na vyuo vya Elimu ya Juu hapa nchini.

Imetolewa na:



Prof. Charles D. Kihampa

**KATIBU MTENDAJI**  
**TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA**